

## 2 Yohana

### *Salamu*

<sup>1</sup> Mzee:

Kwa bibi mteule na watoto wake, niwapendao katika kweli, wala si mimi tu, bali na wale wote waijuayo kweli:

<sup>2</sup> kwa sababu ya ile kweli ikaayo ndani yetu na ambayo itaendelea kukaa nasi milele:

<sup>3</sup> Neema, rehema na amani itokayo kwa Mungu Baba na kwa Yesu Kristo, Mwanawe Baba, itakuwa pamoja nasi katika kweli na upendo.

### *Kweli Na Upendo*

<sup>4</sup> Imenipa furaha kuu kuona baadhi ya watoto wako wanaenenda katika kweli, kama vile Baba alivyotuagiza.

<sup>5</sup> Sasa, bibi mpPENDWA, si kwamba ninakuandikia amri mpya, bali ile tuliyokuwa nayo tangu mwanzo. Tupendane kila mmoja na mwenzake.

<sup>6</sup> Hili ndilo pendo, kwamba tuenende sawasawa na amri zake. Hii ndiyo amri yake kama vile mlivyoSikia tangu mwanzo, kwamba mwenende katika upendo.

<sup>7</sup> Wadanganyifu wengi, wasiokubali kwamba Yesu Kristo amekuja katika mwili, wametokea ulimwenguni. Mtu wa namna hiyo ni mdanganyifu na mpinga Kristo.

**8** Jihadharini msije mkapoteza kile mlichokitenda, bali mpare kupewa thawabu kamilifu.

**9** Mtu yejote asiyedumu katika mafundisho ya Kristo, bali akayaacha, yeje hana Mungu. Yeyote anayedumu katika mafundisho ana Baba na Mwana pia.

**10** Msimpokee mtu yejote anayewajia ambaye hawaletei mafundisho haya, wala msimkaribishe nyumbani mwenu.

**11** Yeyote amkaribishaye mtu wa namna hiyo anashiriki katika matendo maovu ya mtu huyo.

### *Salamu Za Mwisha*

**12** Ninayo mengi ya kuwaandikia, lakini sitaki kutumia karatasi na wino. Badala yake, nataraji kuja kwenu na kuongea nanyi ana kwa ana, ili furaha yetu ipate kuwa timilifu.

**13** Watoto wa dada yako mteule wanakusalimu. Amen.

**Biblica® Toleo Wazi Neno: Bibilia Takatifu™  
Swahili: Biblica® Toleo Wazi Neno: Bibilia  
Takatifu™ (Bible)**

copyright © 2018 Biblica, Inc.

Language: Kiswahili

Translation by: Biblica, Inc.

This translation is made available to you under the terms of the Creative Commons Attribution Share-Alike license 4.0.

You have permission to share and redistribute this Bible translation in any format and to make reasonable revisions and adaptations of this translation, provided that:

You include the above copyright and source information.

If you make any changes to the text, you must indicate that you did so in a way that makes it clear that the original licensor is not necessarily endorsing your changes.

If you redistribute this text, you must distribute your contributions under the same license as the original.

Pictures included with Scriptures and other documents on this site are licensed just for use with those Scriptures and documents. For other uses, please contact the respective copyright owners.

Note that in addition to the rules above, revising and adapting God's Word involves a great responsibility to be true to God's Word. See Revelation 22:18-19.

2021-04-12

---

PDF generated using Haiola and XeLaTeX on 18 Apr 2025 from source files dated 31 Aug 2023

9cbb05be-39f3-5d18-8b2a-4ba788541462